

AFRIPRISE INVESTMENT PLC.

2023 - **2024**

# RIPOTI YA MWAKA

www.afriprise.co.tz

CamScanner

CamScanner

# TAARIFA YA KAMPUNI

*Kwenye Mkutano Mkuu wa 19 wa Wanahisa*

2024

AFRIPRISE INVESTMENT PLC
**MKUTANO MKUU WA**
**19 WA WANAHISA 23-11-2024**

CamScanner

## TAARIFA YA KUITISHA

## MKUTANO NA AKIDI

*Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa.*

*Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasio-pungua 10 wanaomiliki hisa zaidi ya asilimia 50.*

### *TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA*

*Utakaofanyika siku ya jumamosi tarehe 23 Nov 2024.Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa wa wanahisa wa Afriprise Investment Plc, utafanyika siku ya jumamosi tarehe 23 Nov 2024 kwa njia ya mtandao.*

Inapatikana katika tovuti ya Kampuni:
www.afriprise.co.tz



CamScanner

# KUPOKEA AJENDA

*Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama zilivyowasilishwa.*



CamScanner

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 23-11-2024.

Tunapenda kukujulisha kuwa, Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa wa Wanahisa wa AFRIPRISE Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 23-11-2024 kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3:00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidigitali.

## Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa ni:

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa;
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023;
6. Kupokea, Kujadili na Kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2023;
7. Kupokea, Kujadili na Kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2024;
8. Kupokea, Kujadili na Kuridhia Pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
9. Kupokea, kujadili na kuamua Mapendekezo yaliyowasilishwa toka kwa wanahisa;
10. Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi;
11. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Tisa;

## Maelezo:

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 21/11/2024;
2. Taarifa ya Mwaka 2023 na Makabrasha ya Mkutano itapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.afriprise.co.tz) kuanzia tarehe 21/11/2024;
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa, kuteua Mwakilishi atakayehudhuria Mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.afriprise.co.tz). Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe info@afriprise.co.tz au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na. 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 22/11/2024, saa kumi kamili jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu
Tarehe: **23-11-2024**



CamScanner

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05/08/2023 KWA NJIA YA MTANDAO.

## 18.1 WALIOHUDHURIA

**Bwn. Fortunatus Magambo** - Mwenyekiti
**Bwn. Peter Kifunguomali** - Katibu

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 05/08/2023 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 18.2 KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE

Mwenyekiti alifungua Mkutano kwa kuwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wageni Waalikwa na Wafanyakazi wa Kampuni kwenye Mkutano Mkuu wa 18 wa Mwaka. Baada ya Kutolewa taarifa kwamba Akidi ilikuwa imetimia kulingana na Kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni, Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 3:12 Asubuhi.

## 18.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE.

Hakukuwa na Mabadiliko yoyote hivyo Wajumbe walipitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane kama zilivyoainishwa kwenye ajenda.

## 18.4 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA.

Wajumbe walithibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba na zikasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## 18.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA ULIOFANYIKA TAREHE 5 NOVEMBA, 2022.

Taarifa ilitolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba uliofanyika tarehe 5 Novemba, 2022 na kukubaliwa na Wanahisa.

## 18.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022.

**18 .6.1** Wanahisa walipokea taarifa za Mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi Mtendaji na hesabu zilizokaguliwa na kujadili kama ifuatavyo;-

**18.6.2** Waliipongeza Bodi ya Wakurugenzi kwa Taarifa nzuri;



CamScanner

18.6.2.1 Ni vema Bodi iendelee kuangalia namna ya kuongeza mapato ya Kampuni na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima

**18.6.2.2 KUANGALIA FURSA MBALIMBALI KATIKA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA NYINGINE.**

18.6.2.3 Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa, Kampuni imeshachukua hatua ya kuwekeza katika vyanzo vingine vya mapato kama dhamana za serikali za muda mrefu na mfupi.

## 18.7 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA MAHESABU YA KAMPUNI YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022.

Taarifa ya Mahesabu iliwasilishwa na haikukinzana na taarifa nyingine. Kulingana na Taarifa ya mahesabu, shughuli za Kampuni zitaendelea bila kuathiriwa na chochote. Mkaguzi wa Mahesabu aliwajulisha wajumbe kuwa, Kwa mwaka wa fedha wa 2022, Kampuni Ilipata Hati safi. Iliazimiwa kwamba Taarifa ya mahesabu ya Kampuni iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022 imepitishwa kama ilivyowasilishwa.

## 18.8 AZIMIO KUHUSU MALIPO YA GAWIO

Bodi ilipendekeza kuwa malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio. Kwa Wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

Mkutano Mkuu uliazimia na kuridhia gawio la shilingi za Kitanzania (13) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi

## 18.9 UTEUZI WA WAKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA DESEMBA 31, 2023

Bodi ilipendekeza kuwa, CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2023. Ada ya Ukaguzi iliyopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni kabla ya kodi. Ilielezwa kuwa ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

Iliazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2023. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kabla ya kodi kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mahesabu ya Kampuni.



CamScanner

## 18.10 PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kuwa kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2022, Menejimeti ilipendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000), kama ilivyokuwa mwaka jana.

Iliazimiwa kwamba ilivyopendekezwa na Menejimenti malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## 18.11 KUPOKEA, KUJADI LI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA KUBADILISHA JINA LA KAMPUNI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwamba, Bodi inapendekeza kubadili jina na nembo ya Kampuni ili kuimarisha utambulisho wetu, kuzoea mwenendo unaobadilika katika soko na kupata fursa mpya za biashara. .

Bodi ilipendekeza kuwa, Jina la Kampuni liwe ni Afriprise Investment PLC.
Iliazimiwa kwamba Jina la Kampuni na Nembo vibadilike na kuwa AFRIPRISE INVESTMENT PLC.

## 18.13 KUFUNGA KWA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE

Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru wanahisa wote, Wajumbe wa Bodi, Wafanyakazi pamoja na wageni waalikwa wote kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa 18 pamoja na mchango wao katika kuboresha maendeleo ya Kampuni.

Mkutano ulifungwa saa 4:12 Asubuhi

| | |
|---|---|
| ______________________ | ____________________ |
| **Mwenyekiti** | **Katibu** |
| Tarehe: _______________ | Tarehe: _____________ |



CamScanner

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 05/08/2023

### WASILISHO

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 18 uliofanyika tarehe 05, Agosti, 2023 kama kumbukumbu sahihi:-

> **"Azimio la 1/2024**
>
> *Imeazimiwa kuwa muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane uliofanyika tarehe 05/08/2023 ni kumbukumbu sahihi."*



CS CamScanner

Dondoo Na. 19/4/2024


## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

| KUMB | MAELEZO MAFUPI | AZIMIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **18.8** | Malipo ya Gawio | Gawio lilipwe Shilingi Kumi na Tatu (13) kwa kila hisa moja. | Limetekelezwa kwa wale ambao taarifa zao zimekamilika.Walilipwa magawio yao tarehe 07/08/2023. |
| **18.9** | Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu | Mkutano Mkuu uliidhinisha CROWE Tanzania kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2023. | Limetekelezwa. Kampuni ya CroweTanzania ndio wakaguzi wa nje wa hesabu kwa mwaka 2023. |
| **18.10** | Malipo ya Wakurugenzi | Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi 4,800,000 kwa kila mjumbe kwa mwaka 2023. | Malipo ya wakurugenzi kwa mwaka 2023 yalilipwa kiasi cha shilingi 4,800,000. |
| **18.11** | Kubadili Jina la Kampuni | iliazimiwa kwamba Jina la Kampuni na Nembo vibadilike na kuwa AFRIPRISE INVESTMENT PLC. | Limetekelezwa. Jina pamoja na Nembo ya Kampuni vimebadilika na kuwa AFRIPRISE INVESTMENT PLC. |

*Jedwali na. 1*



CamScanner



Dondoo Na. 19/5/2024

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2023.

*Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.*



CamScanner



## TAARIFA YA MWENYEKITI

*"Furaha haipatikani katika kuwa na pesa tu, bali inatokana na mafanikio katika jitihada na ubunifu." - Franklin Roosevelt*

### TAARIFA YA MWENYEKITI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Fedha ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE, zamani Kampuni ya uwekezaji ya TCCIA kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023.

Ninapotafakari kuhusiana na mwaka uliopita, nakumbushwa maneno ya Franklin Roosevelt, yanayosema "Furaha haipatikani katika kuwa na pesa tu, bali inatokana na mafanikio katika jitihada na ubunifu." Mwaka huu, mafanikio yetu hakika yametuletea furaha ya kweli.

Tumepiga hatua kubwa katika ukuaji Pamoja na kujitangaza. Hasa, mafanikio yaliyotokana na utoaji wa hisa za haki ambapo tulifanikiwa kukusanya Tsh bilioni kumi na milioni mia tano (10,500,000,000/=) ambazo zitasaidia kupanua uwekezaji wetu Afrika Mashariki na Kusini.

### BIASHARA ENDELEVU

Biashara endelevu, inabakia kuwa lengo kuu kwa kujitoa na kufanya kazi kwa ufanisi, usalama na uvumbuzi. Kupitia uvumbuzi na kuimarisha ushirikiano, tunalenga maendeleo ya pamoja na endelevu na kutimiza malengo ya wanahisa.

### GAWIO

Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza gawio la Shilingi 13 kwa kila hisa moja kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023. Malipo ya gawio yanategemewa kuidhinishwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

### MATARAJIO YA BAADAYE

Tumejikita kutafuta vyanzo vipya vya mapato na kuboresha ufanisi, tukilenga kujenga ushindani wa kibiashara ambao utaongeza thamani kwa wanahisa wetu.

### SHUKRANI

Nawashukuru Bodi ya Wakurugenzi, wanahisa, wadau, washirika wetu wa kibiashara na timu ya Menejimenti kwa kujitoa kwa pamoja kuhakikisha Kampuni inakua na mafanikio makubwa zaidi.

Ahsanteni sana.

______________________

Fortunatus Makore Magambo
**Mwenyekiti wa Bodi**
Tarehe:..................................



CamScanner



## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

*Mpango Mkakati wetu wa mwaka 2023-2025 umefikia hatua muhimu, kwa kuzingatia matakwa ya wadau, kupata faida, uhakika wa mtiririko wa mapato na ongezeko la mapato. Hii inaenda sawia na lengo letu la kuongezeka kitaifa na kimataifa.*

Peter W. Kifunguomali


## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU


Ninayo furaha kuwasilisha taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji Mkuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023.

## UTANGULIZI

Mpango Mkakati wetu wa mwaka 2023-2025 umefikia hatua muhimu, kwa kuzingatia matakwa ya wadau, kupata faida, uhakika wa mtiririko wa mapato na ongezeko la mapato. Hii inaenda sawia na lengo letu la kuongezeka kitaifa na kimataifa.

## TAARIFA YA KIUTENDAJI

Kampuni imedumisha ukuaji thabiti na ongezeko la mapato na uwekezaji. Taarifa ya kiutendaji na kifedha ya mwaka 2023 pamoja na takwimu linganishi za 2022 zimeainishwa kwenye jedwali hapa chini:

*Jedwali na. 2*

| MAELEZO | 2023 TSH'000' | 2022 TSH'000' |
|---|---|---|
| Mapato ya Jumla katika uendeshaji wa Kampuni | 3,086,834 | 2,997,973 |
| Gharama za Uendeshaji wa Kampuni | 1,049,723 | 1,072,564 |
| Faida baada ya kukata kodi | 1,976,343 | 1,959,810 |
| Mtaji wa Wanahisa | 47,524,928 | 32,329,051 |
| Jumla ya mali za Kampuni | 49,994,556 | 35,216,671 |
| Faida kwa kila hisa | 24 | 25 |




CamScanner

## UWEKEZAJI PAMOJA MAPATO YATOKAYO NA UWEKEZAJI

Kulingana na mpango wetu wa kuwekeza katika maeneo mbalimbali ulileta mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na uwekezaji katika hisa zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Nairobi. Kufikia tarehe 31 Desemba, 2023, Mali zote za Kampuni zilikua na thamani ya TZS 47 bilioni sawa na ongezeko la asillimia arobaini na saba (47%) ikilinganishwa TZS 32 bilioni kufikia tarehe 31 Desemba 2022. Kutokana na hali hiyo, ukuaji wa Kampuni kwa mwaka ni wastani wa 840% (mara 8). Uwekezaji uliongezeka kwa 23% kutoka bilioni 34 tarehe 31 Desemba, 2022. Kutokana na hali hiyo, jumla ya uwekezaji wa Kampuni ni TZS 42 bilioni kufikia tarehe 31 Desemba 2023. Tumewekeza kwenye dhamana za serikali kwa 36%, hisa kwa 61% na 3% kwenye maeneo mengine. Ubora wa Kiutendaji katika Kampuni unachangiwa sana na ufanisi wa uendeshaji wa Kampuni na Mpango Mkakati.

Faida kwa kila hisa ni TZS 24 ikilinganishwa na Shilingi 25 Desemba, 2022 kutokana na uuzwaji wa hisa za haki ambazo ziliongeza idadi ya hisa kwa 100% ikilinganishwa na mwaka jana kama ilivyoelezwa kwenye Kielelezo No. 2

Kutokana na uwekezaji mapato ya Kampuni ni 5% ukilinganisha na 6% Desemba, 2022 kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika, tukitegemea kupata mapato zaidi kwa miaka ijayo. Uwekezaji wa Kampuni na maeneo tulikowekeza kufikia Desemba 31, 2023 umeainishwa kwenye Jedwali hapa chini: (Takwimu zimewekwa kwenye mfumo wa '000')

*Jedwali na. 3*

| AINA YA UWEKEZAJI | 2023 (TSH'000') | % | 2022 (TSH'000') | % |
|---|---|---|---|---|
| Dhamana za Serikali | 15,037,036 | 36 | 13,589,143 | 40 |
| Uwekezaji katika Hisa | 25,357,243 | 61 | 19,626,034 | 58 |
| Uwekezaji wa muda mfupi | 305,000 | 1 | 335,000 | 1 |
| Uwekezaji katika mali zisizohamishika | 221,347 | - | 221,347 | 1 |
| Amana za Makampuni | 750,000 | 2 | 150,000 | - |
| Jumla ya Uwekezaji | **41,671,466** | **100** | **33,921,524** | **100** |

## MTAZAMO WA BIASHARA

Tunategemea kupanua wigo wa uwekezaji katika hisa kutoka Makampuni yaliyoorodheshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Soko la Hisa la Nairobi (NSE) ili kuongeza mapato ya gawio na kukuza mtaji na mapato. Zaidi ya hayo, tunaweka sawia upya uwekezaji wetu katika hisa, dhamana serikali na makampuni na masoko ya kifedha ili kupunguza athari na kuboresha faida. Zaidi ya hayo, tunaendelea kufanya utafiti ili kugundua fursa nyingine za kibiashara.

## HITIMISHO

Ninawashukuru Bodi ya Wakurugenzi, timu ya Menejimenti, Mabenki, Wakaguzi wa mahesabu na wanahisa kwa kuendelea kutuunga mkono. Kwa juhudi zetu pamoja AFRIPRISE itaendelea kustawi.

Ahsanteni sana

..................................................

**Peter William Kifunguomali,**
Afisa Mtendaji Mkuu
Tarehe:

# TAARIFA YA UENDELEVU

Taarifa hii ya uendelevu inaelezea juhudi na mafanikio ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE katika kukuza uendelevu na kuwajibika katika kuendelea na uwekezaji. Kujitoa kwetu kulingana na kanuni za kimazingira, kijamii, na kiutawala (ESG) zinatuongoza katika shughuli zetu na kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji. Taarifa hii inaonyesha hatua muhimu za uendelevu zilizochukuliwa katika mwaka wa kifedha wa 2023.

## Majukumu ya Mazingira

1. Ufanisi wa Nishati
   - Tumefanikiwa kupunguza matumizi ya nishati katika ofisi zetu kwa 15% ikilinganishwa na mwaka uliopita.
   - Uwekezaji wetu unajumuisha Makampuni yanayotunza mazingira vizuri.

2. Kupunguza Taka
   - Matumizi ya digitali yamepunguza matumizi ya karatasi kwa 25%, tukilinganisha na lengo letu la kupunguza athari zetu kwa mazingira.

## Majukumu ya Kijamii

1. Ushirikiano na Jamii
   - Tunazo taratibu za kusaidia jamii ambapo kiasi cha faida zetu tunazopata hutolewa kwa mashirika yanayotoa misaada pamoja na kusaidia miradi ya jamii, inayolenga elimu na afya.
   - Wafanyakazi wetu walishiriki katika kazi za kujitolea, wakisaidia miradi mbalimbali ya kijamii.

2. Ustawi wa Wafanyakazi
   - Tunazo taratibu za upimaji wa afya wa mara kwa mara kwa wafanyakazi wetu, ikijumuisha afya ya akili.
   - Kujitolea kwetu kwa utofauti na ushirikishwaji kunaonekana katika wafanyakazi wetu, ambapo 50% ya wafanyakazi wetu ni wanawake. Pia kuna uwakilishi wa wanawake katika Bodi ya Wakurugenzi.

1. Uwekezaji wa Kimaadili
   - Maamuzi yetu ya uwekezaji yanaongozwa na mfumo dhabiti wa ESG, kuhakikisha kuwa tunaunga mkono biashara zilizo na maadili mazuri.
   - Tunafanya tathmini za mara kwa mara kwa Makampuni tulikowekeza ili kuhakikisha zinazingatia kanuni za mazingira, jamii na Uongozi.

2. Uwazi na Uwajibikaji
   - Tumeanzisha mchakato wa uwazi wa utoaji wa taarifa, tukiwapa wadau taarifa za mara kwa mara kuhusu Maendeleo yetu.

## Malengo ya Uendelevu kwa Mwaka Ujao

1. Mazingira
   - Kupunguza matumizi ya nishati zaidi kupitia mifumo ya usimamizi wa nishati iliyoidhinishwa.



CamScanner

- Kuongeza uwekezaji katika miradi ya nishati mbadala.

2. Kijamii
    - Kuongeza ushirikiano wa kijamii ikiwemo taasisi za elimu ya juu kwa programu zilizofadhiliwa.
    - Kuboresha taratibu zetu za mafunzo kwa wafanyakazi ili kupata fursa bora za kujiendeleza.

3. Uongozi
    - Kuweka mkazo katika kanuni za mazingira, jamii na Uongozi (ESG) zinazotakiwa ikiwemo hatua kali za athari za kijamii.
    - Kuboresha ushirikiano wetu na wadau ili kujumuisha maoni na mapendekezo katika mkakati wetu wa uendelevu.

    Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE imejitolea kuingiza uendelevu katika kila kipengele cha biashara yetu. Tunaamini kuwa uwekezaji dhabiti na mikakati endelevu ni muhimu kwa mafanikio ya muda mrefu na matokeo mazuri kwa jamii. Tunajivunia mafanikio yetu mwaka huu na tutaendelea kujitolea kufikia malengo yetu ya uendelevu katika miaka ijayo.



CamScanner

## TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2023. Taarifa hii inaangazia hali ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023.

## UANZISHWAJI

Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE ilisajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Kampuni imeorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na ipo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## SHUGHULI ZA KAMPUNI

Shughuli kuu za Kampuni ni usimamizi wa uwekezaji, ikilenga uwekezaji katika hisa za Makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, pamoja na amana za muda mfupi za Kampuni ambazo zinatoa faida nzuri, dhamana za serikali na uwekezaji katika maghala yaliyo katika maeneo ya kimkakati. Aidha, Kampuni inawahimiza wanahisa wake kuwa na utamaduni wa kuweka akiba ikiwa na maana ya kuwekeza katika hisa za Kampuni zinazofanya vizuri.
Msingi wa Maadili na Kauli mbiu

## MSINGI WA MAADILI:

- Uwajibikaji,
- Kujitoa,
- Kufanya kazi kwa Pamoja,
- Uaminifu na
- Ubunifu

## MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI

### DHIMA YA KAMPUNI

Kutengeneza ongezeko la thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wa Kampuni kwa kutoa faida nzuri zaidi inayotokana na uwekezaji bora na salama.

### MAONO YA KAMPUNI

Kuwa kituo kikuu cha usimamizi wa uwekezaji Tanzania

### KAULI MBIU

Kwa pamoja tunaweza.
MAADILI KATIKA KAZI:
Uwajibikaji, Kujitoa, Kufanya kazi kwa pamoja, Uaminifu na uvumbuzi.



CamScanner

## TATHMINI YA MATOKEO YA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI

Taarifa za kifedha zimetayarishwa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na matakwa ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sera za uhasibu zimetumika kwa uthabiti ikilinganishwa na mwaka uliopita.
Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023, Kampuni ilipata faida baada ya kodi ya Shilingi 1,976,343,000 ukilinganisha na faida ya Shilingi 1,959,810,000 baada ya kodi ya mwaka uliopita.

Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa 11% kutoka Shilingi 2,997,973,000 mwaka uliopita hadi kufikia Shilingi 3,086,834,000 kwa mwaka mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2023. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na kuongezeka kwa mapato ya gawio kama matokeo ya uamuzi wa Bodi wa kuwekeza katika vyanzo mbalimbali vya mapato.

## MTAJI WA HISA

*Jedwali na. 4*

| | | | IDADI YA HISA | |
|---|---|---|---|---|
| Hisa za Kawaidia | | | **2023** | **2022** |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | | | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 |
| | | | | |
| | **2023** | **2022** | **2023** | **2022** |
| | Shs'000 | Shs'000 | **Idadi ya Hisa** | |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | 2,918,306 | 1,459,153 | 145,915,320 | 72,957,660 |
| Mapato ya Hisa (Share Premium) | 9,828,506 | 708,799 | - | - |
| | **12,746,812** | **2,167,952** | **145,915,320** | **72,957,660** |

Rejea kipengele cha 15 cha Taarifa ya Mahesabu kwa maelezo zaidi ya mwenendo wa wa mtaji wa hisa.

## GAWIO

Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza malipo ya gawio ya Shilingi 13 kwa kila hisa, sawa na Shilingi 1,896,899,160 ukilinganisha na gawio la Shilingi 13 kwa kila hisa, sawa na Shilingi 948,449,580 kwa mwaka 2022.

## MALENGO YA KIMKAKATI

**Ongezeko la thamani:** Kuongeza uwezo wa Kampuni kusimamia Madhubuti matarajio ya wanahisa. Matokeo ya Kimkakati ni pamoja na ongezeko la thamani ya hisa na ukuaji wa Kampuni. Kampuni inalenga kuanzisha Kampuni tanzu na kupanua uwekezaji kutoka uwekezaji wa sasa.

**Uwekezaji Bora;** Lengo ni kuboresha thamani ya Kampuni kupitia rasilimali zetu na kuongeza mapato kupitia uwekezaji. Kampuni inatarajia kuongeza mapato yake kupitia uwekezaji kwa 22% kila mwaka.

**Utendaji Bora;** Kuboresha utendaji kwa wafanyakazi wake waliopo kupitia teknolojia sahihi ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji; kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja, kuongeza utiifu wa taasisi; kuboresha utamaduni wa Kampuni; kuboresha ustawi wa wafanyakazi, na kuongeza ufanisi na tija kwa wafanyakazi. Kampuni inatarajia kufikia uwiano wa ubora wa kiutendaji wa asilimia 95.



CamScanner

## WAKURUGENZI

Wakurugenzi waliopo ofisini tarehe ya kutolewa Taarifa hii ni kama ifuatavyo:

| JINA LA MKURUGENZI | NAFASI | ELIMU | URAIA |
|---|---|---|---|
| Ndg. Fortunatus Makore Magambo | Mwenyekiti | Mchumi | Mtanzania |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Mjumbe | Mchumi | Mtanzania |
| Ndg. Joseph Matanga Kahungwa | Mjumbe | Mhasibu | Mtanzania |
| Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | Kilimo/Mchumi | Mtanzania |
| Ndg. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | Mchumi | Mtanzania |
| Ndg. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | Ununuzi na Ugavi | Mtanzania |
| Ndg. Paul F. Koyi | Mjumbe | TEKNOHAMA | Mtanzania |

Hapakuwa na mabadiliko yoyote ya Wajumbe wa Bodi kwa mwaka 2023.

## MATUKIO BAADA YA KUTOLEWA KWA TAARIFA HII

Hakuna mabadiliko yoyote yaliyojitokeza baada ya tarehe ya kutolewa kwa taarifa hii.

## KATIBU WA BODI

Katibu wa Bodi ya Kampuni hadi tarehe 31 Desemba 2023 alikuwa Ndugu Peter William Kifunguomali.

## MISAADA YA KISIASA NA YA KIJAMII

Kulingana na sera ya Kampuni, hatuchangii michango ya kisiasa. Kwa mwaka 2023 hakukuwa na misaada yoyote iliyotolewa kwenye jamii.

## UDHIBITI WA ATHARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA NA MFUMO WA NDANI

Bodi ina jukumu la mwisho la kusimamia athari zinazoweza kujitokeza na kudhibiti mfumo wa ndani wa Kampuni. Menejimenti inawajibika kuhakikisha mfumo wa utendaji unafanya vizuri. Lengo ni kuhakikisha kuwa mifumo ya kifedha na kiutendaji inaendelea kudhibitiwa na kudumishwa. Lengo kuu ni kutoa uhakika wa mambo yafuatayo:

- Kulinda maslahi ya wanahisa na mali za Kampuni;
- Ufanisi katika Utendaji;
- Kutii Matakwa ya Sheria na Kanuni;
- Upatikanaji wa Taarifa za Mahesabu;
- Kuendelea kwa shughuli za Kampuni katika mazingira ya kawaida na mazingira yenye changamoto.
- Kutoa huduma bora kwa wadau.

Ufanisi wa mfumo wowote wa udhibiti wa ndani unategemea uzingatiaji madhubuti wa hatua zilizowekwa. Kuna athari zinazoweza kujitokeza endapo wafanyakazi watashindwa kuzingatia. Ingawa hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaoweza kutoa uhakika kamili dhidi ya taarifa zisizo sahihi au hasara, mfumo wa Kampuni unategemewa kuwapa wakurugenzi uhakika wa kutosha kwamba taratibu zilizowekwa zinafuatwa kwa ufanisi. Wakurugenzi wamepima mfumo wa udhibiti wa ndani na kwa ujumla wameridhika kama inavyoelezwa hapa chini.

Kampuni ina sera mbalimbali ambazo zinasimamiwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza. Kwa upande mwingine, Kampuni ina huduma ya ukaguzi wa ndani na ya nje ambayo inaripoti kwa Kamati ya Ukaguzi ya Bodi ambapo Bodi inafuatilia na kuelekeza hatua za kurekebisha mazingira ya udhibiti wa ndani.



CamScanner

## TATHMINI YA ATHARI NA UDHIBITI WA NDANI

Kampuni inawekeza katika maeneo yafuatayo:- Taasisi za Kifedha ni pamoja na Dhamana za Serikali, Dhamana za Makampuni, mikopo, Amana za muda maalum za Mabenki na hisa. Lengo kuu ni kuzalisha mapato kwa Kampuni.

## ATHARI KUU ZA KIFEDHA ZINAZOIKABILI KAMPUNI NI PAMOJA NA:

**Athari ya Riba**

Athari ya riba ni athari ya Soko inayotokana na mabadiliko ya bei za hisa ambayo yanaweza kuathiri thamani ya mali za Kampuni. Athari hii inasimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeweka mipaka ya Uwekezaji katika mali zinazobeba athari za riba.

## ATHARI YA HISA KUSHINDWA KUUZWA

Athari ya hisa kushindwa kuuzwa ni athari ya kutokuweza kukidhi mahitaji ya kifedha kwa wakati unaofaa. Kampuni inasimamia athari ya hisa kushindwa kuuzwa kwa kuweka mipango ya fedha inayozingatia malipo ya kifedha yanayotarajiwa na malengo ya biashara. Pia inaweka akiba za kutosha kwa ajili ya matumizi ya dharura.

## ATHARI YA MIKOPO

Athari ya mikopo ni hatari ya kupoteza fedha za Kampuni kutokana na kutokulipwa kwa mikopo au madeni na wateja au watoaji wa huduma. Kampuni ina sera na taratibu za kupima na kudhibiti athari ya mikopo. Inaweka mipaka ya kuhusisha wateja na watoaji wa huduma kulingana na rekodi za malipo na uwezo wao wa kifedha.

## ATHARI ZA UTENDAJI

Athari za utendaji hutokana na mifumo isiyotosheleza, kushindwa kwa usimamizi, michakato isiyo madhubuti ya udhibiti wa ndani, ulaghai, wizi, na makosa ya kibinadamu. Kampuni inashughulikia athari hizi, miongoni mwao ni uhakika wa kuwepo kwa mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani. Vyombo vikuu vya mfumo wa udhibiti wa ndani ni pamoja na miongozo ya utendaji na taratibu, sera na mwongozo, na huduma ya ukaguzi wa ndani na wa nje. Kusimamia athari za uendeshaji ndani ya Kampuni ni sehemu muhimu ya shughuli za kila siku za usimamizi. Usimamizi, huduma ya ukaguzi wa ndani na nje, Kamati ya Ukaguzi, na Bodi ya Wakurugenzi wanahusika kikamilifu katika mchakato wa ufuatiliaji.

## ATHARI ZA RASILIMALI WATU

Asili ya shughuli za Kampuni inahitaji timu yenye taaluma mbalimbali yenye ujuzi maalum katika maeneo muhimu ya uendeshaji. Muundo wa wafanyakazi wachache wa Kampuni unaleta uwezekano mkubwa wa kuondoka kwa wafanyakazi. Ili kushughulikia athari hii, Kampuni inahakikisha kwamba inawekeza katika kujenga uwezo kwa wafanyakazi wake, na kurekebisha muundo wa malipo mara kwa mara.

## ATHARI YA KAMPUNI KUPOTEZA SIFA

Kampuni ina wajibu wa kuhakikisha kwamba inatekeleza majukumu yake na kudumisha sifa yake kama moja ya Kampuni zilizoorodheshwa na zinazofanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazotumika.



CamScanner

Katika jitihada hii, Bodi na Menejimenti wanahakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa kutumia Kanuni za usimamizi bora wa Kampuni na kutumia mbinu bora zaidi.

## IDADI YA HISA ZINAZOMILIKIWA NA WAJUMBE WA BODI KWENYE KAMPUNI

Mpaka kufikia Desemba 31, 2023, idadi ya Hisa za kila Mjumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo:

| | IDADI YA HISA WANAZOMILIKI | |
|---|---|---|
| **WAKURUGENZI** | **2023** | **2022** |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | 131,760 | 65,880 |
| Joseph Matanga Kahungwa | 81,200 | 40,600 |
| Magdalene Nelson Enock Mkocha | 204,724 | 102,363 |
| Nathan Edward Mnyawami | 42,150 | 21,075 |
| Paul Faraji Koyi | 20,000 | - |
| | **479,834** | **229,918** |

Bodi ya Wakurugenzi pia inajumuisha Wakurugenzi wanaowakilisha mashirika yanayomiliki hisa katika Kampuni. Wakurugenzi hawa ni kama ifuatavyo:

- Paul F. Koyi, Rais wa TCCIA - anayewakilisha Makao Makuu ya TCCIA na Ofisi za Mikoa ambazo zinamiliki jumla ya hisa 792,492.

- Fortunatus Magambo na Ernest R. Khisombi - wote wawili wakiwakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ambao unamiliki jumla ya hisa 65,661,894.

## UONGOZI BORA

Bodi inawajibika kwa wajibu wote wa Kampuni. Hii inajumuisha, kati ya mambo mengine, kutambua athari ambazo zinaweza kuathiri vibaya shughuli za Kampuni, kwa kuzingatia na kufuatilia maamuzi makubwa ya uwekezaji. Bodi pia inawajibika kuhakikisha kuwa sera na taratibu za kina za udhibiti wa ndani zipo, zinatumika kwa ufanisi na zinafuata kanuni zinazokubalika za utawala bora wa Kampuni.

Katika mwaka uliopita, Bodi ilikutana mara sita (6), ambapo mikutano minne (4) ilikuwa mikutano ya kawaida na mikutano miwili (2) ilikuwa mikutano ya dharura iliyofanyika kwa lengo la kushughulikia shughuli maalum ambazo zilihitaji umakini wa Bodi. Bodi imemkabidhi Mkurugenzi Mtendaji jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za Kampuni ambaye anasaidiwa na timu ya Menejimenti. Menejimenti wanaalikwa kuhudhuria mikutano ya Bodi na kuwezesha udhibiti mzuri wa shughuli za Kampuni. Mikutano ya dharura ilijumuisha majadiliano na kuidhinishwa kwa mpango wa mwaka na bajeti, na Mahesabu yaliyokaguliwa ya mwaka.

## WAJUMBE WA BODI NA IDADI YA VIKAO WALIVYOHUDHURIA MWAKA 2023

| NA. | JINA | NAFASI | IDADI YA VIKAO | IDADI YA VIKAO ALIVYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Fortunatus M. Magambo | Mwenyekiti | 6 | 6 |
| 2. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 6 | 6 |
| 3. | Bw. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 6 | 6 |
| 4. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 6 | 6 |
| 5. | Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 6 | 6 |
| 6. | Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe | 6 | 1 |
| 7. | Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 6 | 6 |



CamScanner

Wakurugenzi wote wana tabia njema na wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu, maamuzi, na hawana uhusiano au hali zinazoweza kuathiri maamuzi yao. Wakurugenzi wote wanafanya kazi kwa maadili katika kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu.

Wakurugenzi wote wana sifa na uzoefu unaojitegemea ambao unasaidia katika kufanya maamuzi.

Bodi inatambua na imejitolea na inafuata Kanuni za Uongozi Bora wa Kampuni. Katika mwaka uliopita, Bodi ilitumia Kamati mbili za bodi ili kuwezesha kufikia viwango vya juu vya utawala Bora wa Kampuni na pia kuchukua maamuzi kwa wakati kuhusu masuala yahusuyo Kampuni. Kamati hizo mbili zilikuwa:

- Kamati ya Uwekezaji, ambayo inaundwa na Wajumbe watatu.
- Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Athari, ambayo inaundwa na Wajumbe watatu.

| WAJUMBE WA KAMATI YA UWEKEZAJI NI HAWA WAFUATAO | | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe |
| 3. | Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe |

Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara nne (4) kujadili taarifa za utendaji za kila robo mwaka na pendekezo la uwekezaji kabla ya kuwasilisha taarifa hizo kwenye Bodi kwa ajili ya majadiliano na uamuzi.

| WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA ATHARI | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Joseph M. Kahungwa | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe |
| 3. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe |

Kamati ilikutana mara sita (6) kujadili na kupitisha taarifa za ukaguzi wa ndani za kila robo mwaka ambazo ziliandaliwa na Mkaguzi wa Ndani na pia kupitia mahesabu ya Kampuni ya mwaka mzima yaliyokaguliwa.

## SHUGHULI KUU ZILIZOFANYWA NA BODI MWAKA 2023

Mbali na kutekeleza shughuli za kawaida za kusimamia uendeshaji wa Kampuni, Bodi pia ilishughulikia masuala yafuatayo:

- Kukagua na kuidhinisha suala la Uuzwaji wa Hisa za Haki;
- Kukagua na kuidhinisha jina Jipya la Kampuni;
- Kuhakiki taarifa za Wahanisa;
- Kukagua ripoti za ndani za ukaguzi wa Kampuni za robo mwaka;
- Kukagua njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza mapato;
- Maandalizi na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka na bajeti ya mwaka 2023;
- Kuchambua taarifa mbalimbali za uwekezaji na kutafuta fursa mpya za biashara.



CamScanner

## UZINGATIAJI WA SHERIA NA KANUNI

Kampuni imeendelea kudumisha uhusiano mzuri na wadau wake muhimu. Kampuni pia ilidumisha uhusiano mzuri na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Soko la Hisa la Dar es Salaam, Madalali na benki za kibiashara. Kwa mwaka 2023, Kampuni ilizingatia sheria na miongozo yote iliyotolewa na mamlaka mbalimbali za udhibiti.

Usahihi wa Kumbukumbu za Kihasibu na Taarifa za Mahesabu

Kampuni ina wafanyakazi wenye ujuzi katika Idara ya Uhasibu na Fedha. Kwa hivyo, vitabu vya hesabu vinahifadhiwa kwa usahihi na Taarifa za kifedha zimeandaliwa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IFRS).

## MUUNDO WA MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji ulioidhinishwa wa Kampuni ni Shilingi 100,000,000,000 uliogawanywa katika hisa zenye thamani ya Shilingi 20 kama ilivyokuwa tarehe 31 Desemba 2023. Mtaji uliolipiwa wa Kampuni unaojumuisha hisa za kawaida mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ulikuwa Shilingi 12,746,812,000.

| | | |
|---|---|---|
| Hisa za Kawaida 145,915,320 | | |
| (2022:72,957,660) zenye thamani ya Shilingi 20/- kila hisa moja | 2,918,306 | 1,459,153 |
| Mapato katika Hisa (Share Premium) | 9,828,506 | 708,799 |
| **Mtaji Uliolipiwa** | **12,746,812** | **2,167,952** |

| MUUNDO WA UMILIKI WA HISA | ASILIMIA | SHS'000 |
|---|---|---|
| PSSSF | 45 | 1,313,238 |
| Abbasi Export Ltd | 13 | 387,746 |
| Joyce Mwita Gachuma | 5 | 150,000 |
| Christopher Mwita Gachuma | 2 | 116,732 |
| Amin Mohamed Valji | 2 | 42,200 |
| Wanahisa wengine (chini ya 1.5) | 31 | 908,390 |
| | **100** | **2,918,306** |

## TAARIFA ZA SOKO LA HISA

Kampuni imesajiliwa Kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Bei ya hisa kama ilivyokuwa tarehe 31 Desemba 2023 ilikuwa Shilingi 190 ukilinganisha na Shilingi 155 kwa mwaka 2022 na mtaji wa Soko ulikuwa ni Shilingi 27,723,911,000 ukilinganisha na Shilingi 11,330,000,000 kwa mwaka 2022.

## BIASHARA ENDELEVU

Majadiliano ya Wakurugenzi kuhusu kuendelea kwa biashara hayazingatii tu taarifa za Kifedha. Bodi inachukulia kuwa ni muhimu kufuatilia na kujua masuala mapana ya uendelevu wa biashara, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na upatikanaji wa rasilimali kwa njia zenye manufaa ili biashara yetu iweze kufanikiwa katika miaka ijayo. Pia tunaamini katika kukuza miradi endelevu inayozingatia mazingira



CamScanner

kwa kuepuka kufadhili/miradi, biashara, ambazo zinaweza kuwa tishio kwa mazingira licha ya ufanisi wao wa kifedha, tunawahimiza wafanyakazi na wadau wengine kuendeleza, kuhamasisha na kukuza matumizi ya Teknolojia rafiki kwa mazingira; Tunahimiza AFRIPRISE kukumbatia biashara kupitia mifumo, tunajenga mtazamo miongoni mwa wafanyakazi wa kuhamasisha, kuwahimiza wadau kupitia uanzishaji wa mfumo sahihi wa usimamizi wa athari za mazingira kupitia kuanzishwa kwa teknolojia sahihi, tunakuza programu za uhamasishaji kwa teknolojia rafiki kwa mazingira kupitia utekelezaji wa Uwajibikaji wa Kijamii wa Kampuni (CSR).

## KUENDELEA KWA SHUGHULI ZA KAMPUNI

Wakurugenzi wanaamini kuwa Kampuni ina rasilimali za kutosha kuendelea na shughuli za kibiashara kwa siku zijazo na kwa hivyo taarifa za kifedha zimeandaliwa kwa msingi wa biashara endelevu. Wakurugenzi wamejiridhisha kuwa Kampuni ipo katika hali nzuri ya kifedha na ina uwezo wa kupata mikopo ya kutosha kukidhi mahitaji yake ya fedha yanayotarajiwa. Wakurugenzi hawajui mabadiliko mapya yoyote ya muhimu ambayo yanaweza kuathiri vibaya Kampuni. Wakurugenzi pia hawajui kuhusu kutokuzingatia kwa sheria au kanuni zozote au mabadiliko yanayokuja katika sheria ambazo zinaweza kuathiri Kampuni.

## USTAWI WA WAFANYAKAZI

Kampuni ina mipango ifuatayo ya kuendeleza  wafanyakazi wake:

## MAFUNZO

Kampuni inatoa udhamini kwa wafanyakazi wake katika mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi katika taaluma mbalimbali kulingana na mahitaji ya Kampuni na rasilimali za kifedha zinazopatikana. Kampuni pia inaunga mkono juhudi binafsi za wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mrefu.

## MIKOPO NA MALIPO YA AWALI KWA WAFANYAKAZI

Kampuni hutoa malipo ya awali ya mshahara kuwasaidia wafanyakazi kukidhi mahitaji ya kifedha na kukuza maendeleo yao ya kiuchumi. Malipo ya awali ya mshahara hutolewa kwa masharti maalum yaliyoidhinishwa na Bodi na hutolewa kwa mujibu wa bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa.

## MSAADA WA KIFEDHA

Kampuni ina sera ya kusaidia katika tukio la kifo cha mfanyakazi au mtegemezi wa familia wa karibu.

## MALIPO YA KUSTAAFU

Kampuni huchangia mifuko ya hifadhi ya jamii inayosimamiwa na umma ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa niaba ya wafanyakazi wote.

## WATU WENYE ULEMAVU

Kampuni inatoa nafasi sawa kwa watu wenye ulemavu kwa nafasi wanazoweza kujaza kwenye Kampuni



CamScanner

## HUDUMA ZA MATIBABU

Kampuni imeingia mkataba na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutoa huduma ya matibabu kwa wafanyakazi wake na wategemezi wa karibu.

### USAWA WA KIJINSIA

Kama ilivyokuwa tarehe 31 Desemba 2023, Kampuni ilikuwa na wafanyakazi sita, kati ya hao watatu walikuwa ni wanaume na watatu walikuwa ni wanawake, idadi ambayo ni sawa na ile ya mwaka 2022.

### MASUALA YA MAZINGIRA, KIJAMII NA UONGOZI

Kampuni inakua makini katika masuala ya Mazingira, Kijamii na Uongozi na tumejifunza njia bora za kupima kile ambacho tumekuwa tukikifanya. Kampuni imejizatiti kwenda "kijani" kwa kufanya kazi katika mazingira yasiyohitaji karatasi na kuwekeza mitaji yetu katika Kampuni zinazozingatia sheria za mazingira na usalama.

### SHUGHULI ZA BAADAYE ZA MAENDELEO

Tangu mwaka 2018 Wakurugenzi waliamua kuanza taratibu kubadili mwelekeo wa uwekezaji wa Kampuni kwa kuwekeza katika maeneo mengine ambayo ilikua haijawekeza hapo awali. Tangu Kampuni ilipoanza shughuli zake za biashara mwezi Oktoba, 2005, zaidi ya 95% ya uwekezaji wake ulikuwa katika hisa za makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Bodi iliamua kulenga uwekezaji katika taasisi za kifedha zenye mapato ya kudumu (hatifungani za serikali, dhamana za muda mfupi, na amana za benki zinazotoa riba).

Wakurugenzi wanaamini kuwa uwekezaji katika taasisi hizi, unaileteа Kampuni mapato ya kudumu na kupata faida nzuri hasa wakati Soko la Hisa halifanyi vizuri kama ilivyo sasa ambapo mapato ya uwekezaji huu sio ya uhakika. Hata hivyo, Bodi imeamua kuendelea na njia hii ya uwekezaji, hasa kwa sababu mapato ni ya kuvutia na ni ya uhakika zaidi kuliko katika mapato ya gawio.
Mwisho, Bodi inaendelea kuchunguza fursa nyingine za biashara ikiwa ni pamoja na biashara ya kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, biashara ya mifugo, na bidhaa zingine za kifedha kama vile biashara ya hati fungani.

### ULINZI WA MALI ZA KAMPUNI

Wakurugenzi wanawajibika kwa kulinda mali za Kampuni. Bodi imeidhinisha sera na kanuni mbalimbali zikiwemo kanuni za kifedha, na sera ya uwekezaji ili kuimarisha mazingira ya udhibiti wa ndani. Hizi zinapitiwa mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya uendeshaji. Wakurugenzi wanapenda kutoa taarifa kuwa wakati wa mwaka uliopita hakukuwa na matukio makubwa ya udanganyifu yaliyoripotiwa.



CamScanner

**MAMBO YAHUSUYO MIAMALA**

Mambo yote yahusuyo miamala yameainishwa katika kifungu Na. 34 cha Taarifa ya Fedha.

**WAJIBU WA WAKURUGENZI**

Ni jukumu la Wakurugenzi kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha zinaonyesha hali halisi ya Kampuni mwishoni mwa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli zake na mtiririko wa fedha kwa kipindi kilichomalizika, kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya uaandaji wa taarifa ya Fedha na sheria, kanuni na masharti yanayotumika. Wakurugenzi pia wanathibitisha kufuata masharti ya mahitaji ya Kiwango cha kutoa taarifa ya fedha cha Tanzania 1 (TFRS 1) na sheria nyingine zote zinazohusiana na Kampuni.

## WAKAGUZI

Wakaguzi wa Kampuni, Crowe Tanzania, wameonyesha utayari wao wa kuendelea kufanya kazi na Kampuni na wanastahili kuteuliwa tena kukagua taarifa za kifedha kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2024. Pendekezo hili litawasilishwa kwenye mkutano kwa majadiliano na kuidhinishwa.

## MKUTANO MKUU.

Taarifa za kifedha zilizowekwa kwenye ukurasa wa 22 hadi 63, ambazo zimetayarishwa vizuri, ziliidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe ya taarifa hii, na zilisainiwa kwa niaba Bodi na:

Fortunatus Makore Magambo
**Mkurugenzi**

**Tarehe:** 25 Juni 2024

Prof. Lucian Ambrose Msambichaka
**Mkurugenzi**

**Tarehe:** 25 Juni 2024

# TAARIFA YA MKUU WA IDARA YA UHASIBU WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE PLC

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu Na. 33 ya mwaka 1972, na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya mwaka 1995, inahitaji taarifa za kifedha kuambatanishwa na tamko lililotolewa na Mkuu wa Idara ya Uhasibu anayehusika na maandalizi ya taarifa za kifedha za taasisi husika.

Ni jukumu la Mhasibu Mtaalamu kusaidia Bodi ya Wakurugenzi/Mamlaka ya Uongozi/Menejimenti kutekeleza jukumu la kuandaa taarifa za kifedha za taasisi zinazoonyesha hali halisi ya utendaji wa taasisi kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu vinavyotumika na mahitaji ya kisheria ya utoaji wa taarifa za kifedha.

Jukumu kamili la kisheria la kuandaa taarifa za kifedha linabaki kwa Bodi ya Wakurugenzi/Mamlaka ya Uongozi kama ilivyoelezwa chini ya Taarifa ya Majukumu ya Wakurugenzi kwenye ukurasa wa awali.

Mimi, Joel Chikoma, nikiwa Mkuu wa Idara ya Uhasibu ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE tarehe 31 Desemba 2023 na kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, ninatambua jukumu langu la kuhakikisha kuwa taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2023 zimeandaliwa kwa kufuata viwango vya uhasibu vinavyotumika na matakwa ya kisheria.

Hivyo, nakiri kuwa taarifa za fedha zinatoa taswira halisi na haki ya hali ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kama ilivyokuwa tarehe hiyo na kwamba zimeandaliwa kwa msingi wa kumbukumbu za kifedha zilizohifadhiwa vizuri.

Jina: **Joel Chikoma**

Sahihi:

Nafasi: **Head of Finance**

NBAA Membership No: **ACPA 3285**

**Tarehe:** 25 Juni 2024



CS CamScanner

# TAARIFA YA MAHESABU



## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

## YA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2023

| | 2023<br>Shilingi' 000 | 2022<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| Mapato | 3,086,834 | 2,997,973 |
| Mapato anuwai | 159,304 | 256,091 |
| Mapato mengine/ (hasara) ya uendeshaji | 184,951 | 154,457 |
| Matumizi ya uendeshaji | (1,049,723) | (1,072,564) |
| **Faida ya uendeshaji** | **2,381,366** | **2,335,957** |
| Gharama za kifedha | (345,233) | (349,966) |
| **Faida/ (hasara) kabla ya kodi** | **2,036,133** | **1,985,991** |
| Kodi | (59,790) | (26,181) |
| Faida/(Hasara) kwa mwaka | **1,976,343** | **1,959,810** |
| **Mapato mengine kamili:** | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | 4,181,980 | 3,839,666 |
| **Mapato/(hasara) mengine ya mwaka** | 4,181,980 | 3,839,666 |
| **Jumla ya mapato/(hasara) kwa mwaka** | **6,158,323** | **5,799,476** |
| **Faida kwa kila hisa** | **23.71** | **25.23** |



CamScanner

# TAARIFA YA WARAKA KAMA
# ILIVYOKUWA HADI TAREHE 31/12/2023

| | 2023 Shilingi' 000 | 2022 Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali** | | |
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 109,068 | 117,257 |
| Uwekezaji wa kwenye ardhi/majengo | 221,347 | 221,347 |
| Haki ya matumizi ya rasilimali | 59,711 | 31,050 |
| Rasilimali zisizogusika | 3,040 | 3,000 |
| Mikopo | 73,173 | 28,734 |
| Uwekezaji wa kwenye hisa | 25,357,243 | 19,626,034 |
| Dhamana za serikali | 15,037,876 | 13,589,143 |
| Uwekezaji mwingine wa kifedha | 600,000 | 150,000 |
| | **41,461,458** | **33,766,565** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Mikopo | 28,954 | 32,994 |
| Rasilimali za biashara | 1,036,105 | 599,931 |
| Kodi ya muda mfupi | 308,164 | 286,996 |
| Uwekezaji mwingine wa kifedha | 455,000 | 335,000 |
| Fedha na thamani ya fedha | 6,704,875 | 195,185 |
| | **8,533,098** | **1,450,106** |
| **Jumla ya Rasimali** | **49,994,556** | **35,216,671** |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| Mtaji | 12,746,812 | 2,167,952 |
| Jumla ya akiba | 12,559,826 | 8,883,288 |
| Faida kuu | 22,218,290 | 21,277,811 |
| | **47,524,928** | **32,329,051** |
| **Madeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | 1,885,443 | 2,157,861 |
| Dhima ya kukodisha | 32,944 | - |
| Kodi iliyoahirishwa | 1,784 | 1,784 |
| | **1,920,171** | **2,159,645** |
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Madeni ya biashara | 200,758 | 127,863 |
| Mkopo wa muda mfupi | 272,398 | 239,081 |
| Gawio | 51,922 | 330,428 |
| Dhima ya kukodisha | 24,379 | 30,603 |
| | **549,457** | **727,975** |
| **Jumla ya madeni** | **2,469,628** | **2,887,620** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **49,994,556** | **35,216,671** |



CamScanner

# TAARIFA YA MABADILIKO
# YA MTAJI KWA MWAKA 2023

| | Mtaji wa hisa Shilingi' 000 | Mapato ya hisa 000' | Jumla ya mtaji wa hisa 000' | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa 000' | Gharama uuzaji wa hisa 000' | Faida kuu 000' | Jumla ya mtaji 000' |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| <u>Mwaka uliopita</u> | | | | | | | |
| **Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 1/1/2022** | 1,459,153 | 708,799 | 2,167,952 | 5,957,424 | (629,662) | 19,908,600 | 27,404,314 |
| Faida ya mwaka | | | | | | 1,959,810 | 1,959,810 |
| Mapato mengine | | | | 3,839,666 | | | 3,839,666 |
| Kuhamisha kwenda akiba kuu | | | | (284,140) | | 284,140 | - |
| Gawio | | | | | | (729,577) | (729,577) |
| Kodi ya zuio miaka ya nyuma | | | | | | (145,162) | (145,162) |
| **Mtaji wa hisa kuanzia 31/12/2022** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **9,512,950** | **(629,662)** | **21,277,813** | **32,329,053** |
| <u>Mwaka huu</u> | | | | | | | |
| **Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 1/1/2023** | 1,459,153 | 708,799 | 2,167,952 | 9,512,950 | (629,662) | 21,277,813 | 32,329,053 |
| Faida ya mwaka | | | | | | 1,976,343 | 1,976,343 |
| Mapato mengine | | | | 4,181,980 | | | 4,181,980 |
| Mauzo ya hisa za upendeleo | 1,459,153 | 9,119,707 | 10,578,860 | | | | 10,578,860 |
| Gharama za mauzo ya hisa | | | | | (599,426) | | (599,426) |
| Kuhamisha kwenda akiba nyingine | | | | 93,984 | | (87,416) | 6,568 |
| Gawio | | | | | | (948,450) | (948,450) |
| **Mtaji wa hisa kuanzia tarehe 31/12/2023** | **2,918,306** | **9,828,506** | **12,746,812** | **13,788,914** | **(1,229,088)** | **22,218,290** | **47,524,928** |



CamScanner

# TAARIFA YA

# MTIRIRIKO WA FEDHA

| | 2023<br>Shilingi' 000 | 2022<br>Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | | |
| Fedha toka kwenye shughuli za uendeshaji | 1,296,072 | 2,080,332 |
| Gharama za kifedha | (345,233) | (349,966) |
| Kodi iliyolipwa | (80,958) | (92,602) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **869,881** | **1,637,764** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (16,928) | (10,567) |
| Manunuzi ya Haki ya kutumia Rasilimali | (57,323) | (57,323) |
| Manunuzi ya Rasilimali Isiyogusika | (2,053) | - |
| Manunuzi ya amana za serikali | (1,549,229) | (527,028) |
| Mtiririko kwenye uwekezaji katika hisa | (3,214,829) | (1,009,953) |
| Mikopo | (40,399) | (61,728) |
| Manunuzi ya uwekezaji mwingine wa kifedha | (570,000) | (135,000) |
| Mauzo ya uwekezaji katika hisa | 1,951,047 | 560,371 |
| **Fedha taslimu iliyotumika katika uwekezaji** | **(3,499,714)** | **(1,241,228)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na mtaji** | | |
| Mauzo ya hisa za upendeleo | 10,578,860 | - |
| Mtiririko wa mkopo | (239,101) | (209,251) |
| Mtiririko wa dhima ya kukodisha | 26,720 | 30,603 |
| Gawio lililolipwa | (1,226,956) | (684,002) |
| **Fedha taslimu iliyotokana na mtaji** | **9,139,523** | **(862,650)** |
| **Jumla ya fedha taslimu za Mtiririko kwa mwaka** | 6,509,690 | (466,114) |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | 195,185 | 661,299 |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **6,704,875** | **195,185** |



CamScanner

WEKEZA

SASA NA

AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.



Dondoo Na. 19/5/2024

## WASILISHO

**WASILISHO:**

Ndugu Wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023 na kuazimia kama ifuatavyo.

# Azimio la 2/2024

*"Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2023 imepitishwa kama ilivyowasilishwa."*





CamScanner

# KUTANGAZA GAWIO

## KUTANGAZA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba, 31 2023, Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 13 kwa hisa, ambayo ni sawa na kiasi kilicholipwa mwaka 2022 cha shilingi 13 kwa hisa.

## WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.



**“Azimio la 3/2024**

*Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Kumi na tatu (13) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.”*

## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2024

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2023, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2023. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

**WASILISHO**

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2024. Ada ya ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 22 milioni Kabla ya kodi. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

## Azimio la 4/2024

*"Imeazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2024. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 22 milioni kabla ya kodi kama gharama za malipo ya ukaguziwa Mahesabu ya Kampuni."*

## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi.


Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2023, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni sita na laki mbili (Shilingi 6,200,000).

## Azimio la 5/2024

*"Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni sita na laki mbili (Shilingi 6,200,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi."*



## PENDEKEZO LA KUPUNGUZA IDADI YA WAJUMBE WA BODI

Tulipokea barua kutoka PSSSF ikieleza pendekezo la kupunguza idadi ya Wajumbe pamoja na kuainisha uwakilishi wa nafasi kwenye Bodi kulingana na muundo wa hisa za Kampuni kwa sasa baada ya zoezi la uuzwaji wa hisa za upendeleo.
Sababu kubwa ya kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi ni kuipunguzia Kampuni gharama za uendeshaji husussan zile zinazotokana na Mikutano ya Bodi pamoja na Kamati zake.

### MAPENDEKEZO YA PSSSF.

Kupunguza idadi ya Wajumbe wa Bodi kutoka saba (7) mpaka watano (5). Pendekezo hili kama likikubaliwa na Mkutano Mkuu hakutakua na haja ya kufanya Mabadiliko kwenye Katiba ya Kampuni (Memorandum of Articles of Association). Hii ni kwa sababu Kampuni itabaki na idadi ya chini ambayo inatamkwa kwenye Katiba ya Kampuni (MEMARTS).

Kuainisha uwakilishi wa nafasi kwenye Bodi kulingana na muundo wa hisa za Kampuni kwa sasa baada ya zoezi la uuzwaji wa hisa za upendeleo.

Wanahisa ambao wanamiliki asilimia arobaini na tano (45%) au zaidi watengewe nafasi mbili kwenye Bodi na wale wanaomiliki kati ya asilimia kumi na tano (15%) mpaka ishirini na tisa (29%) watengewe nafasi moja na nafasi Mbili watengewe wanahisa wadogo.

## *Azimio la 6/2024*

***AZIMIO LA BODI***
***Mkutano Mkuu uridhie***

- *Idadi ya wajumbe wa Bodi iwe watano (5).*
- *Wanahisa ambao wanamiliki asilimia arobaini na tano (45%) au zaidi watengewe nafasi mbili na wale wanaomiliki kati ya asilimia kumi na tano (15%) mpaka ishirini na tisa (29%) watengewe nafasi moja na nafasi mbili (2) watengewe wanahisa wadogo.*
- *Wakati wa kupiga kura kuchagua Wawakilishi wa Wanahisa wadogo ambao Kundi ambalo limetengewa nafasi ya uwakilishi halitashiriki kupiga kura.*
- *Wakati wa kupiga kura, kila hisa moja itakuwa sawa na kura moja.*





CamScanner

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI

### 1. UTANGULIZI

1.1 Kifungu Namba 69 cha Katiba ya Kampuni, kinatamka kuwa, idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi itakuwa si chini ya 5 wala haitazidi 7 kama ifuatavyo:.

1.1.1 PSSSF nafasi mbili (2), TCCIA nafasi moja (1) na nafasi nne (4) wanahisa wengine.

### 2. SIFA ZA MWOMBAJI.

2.1 Mwombaji awe ni mwanahisa wa Kampuni.

2.2 Mwombaji awe na elimu ya Chuo Kikuu au elimu ya juu kutoka Chuo chochote kinachotambulika kitaifa au kimataifa, mwenye elimu ya uchambuzi na ufahamu wa kina katika masuala ya kitaaluma kama vile: Uhasibu, Kilimo, Biashara, Sheria, Uwekezaji, Uchumi, Fedha na Utawala.

2.3 Awe na uwezo wa kujieleza kwa Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.

2.4 Mwombaji awe na uzoefu wa Ukurugenzi kwenye Bodi za makampuni kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu.

### 3. HATUA ZILIZOCHUKULIWA.

3.1 Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuavyo:

3.1.1 Tarehe 30/09/2024, Tangazo lilitolewa kwa ajili ya kujaza nafasi nne (4) zilizobaki baada ya kutenga nafasi 2 kwa ajili ya PSSSF na nafasi 1 kwa ajili ya TCCIA. Tangazo lilielekeza kwamba maombi yawasilishwe kabla ya tarehe 11/10/2024. Tangazo hili lilitangazwa kwenye gazeti Citizen na kwenye mitandao ya kijamii.

3.1.2 Katika kuzingatia kuwa tathmini inafanyika kwa uhuru na haki Bodi iliteua Menejimenti kufanya tathmini ya maombi na kuwasilisha mapendekezo yake mbele ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa ajili ya uchaguzi. Maombi yaliyopokelewa ni yale yaliyowasilishwa kulingana na muda uliokuwa umewekwa kama inavyoonyeshwa kwenye tangazo.

### 4. MWISHO

4.1 Mwisho Mkutano Mkuu unaombwa kupokea orodha ya Wajumbe waliokidhi vigezo kuwa Wajumbe wa Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu (3) ijayo, kuanzia 23/11/ 2024. Baada ya hapo Mkutano Mkuu uhitimishe zoezi kwa kupiga kura.

4.2 Mkutano Mkuu upokee na kuridhia Wajumbe wawili walioteuliwa kutoka PSSSF na mjumbe mmoja ambaye ni Raisi wa Chemba anaewakilisha Wanahisa wadogo (Minorite Shareholders).

4.3 Wakati wa kupiga kura, kila hisa moja ni sawa na kura moja.



CamScanner

## WASIFU WA WAGOMBEA



### 1. NATHAN EDWARD MNYAWAMI

Bwana Mnyawami ana Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Makerere (1993) na Shahada ya Uzamili ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2002). Ana uzoefu wa miaka 20 katika kazi mbalimbali. Aliwahi kuajiriwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kama Mtakwimu chini ya Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji kuanzia 1994 hadi 2002. Mwaka 2002 hadi 2015, alijiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mashirika ya Umma (PPF) kama Meneja wa Mipango na Utafiti. Mwaka 2015 alirudi TPDC kama Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji. Bwana Mnyawami ana uzoefu wa zaidi ya miaka 10 katika uanachama wa bodi mbalimbali na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).



### 2. PROF. LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA

Prof. Msambichaka ana Shahada ya Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada za Uzamili na Uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Leipzig, Ujerumani. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 10 katika uanachama wa bodi mbalimbali kama vile Jumuiya ya Uchumi ya Kilimo Tanzania, Jumuiya ya Uchumi Tanzania, na ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji. Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi za taasisi kama Bodi ya Wakurugenzi ya Ngozi Morogoro, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa, na Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA). Pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).



### 3. JOSEPH MATANGA KAHUNGWA

Bwana Kahungwa ana Shahada ya Biashara katika Uhasibu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1987) na Shahada ya Uzamili katika Uongozi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2003). Amehudumu kama Makamu wa Rais (Kilimo) wa TCCIA tangu Mei 2013. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 10 katika uanachama wa bodi, na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).



CamScanner



**4. MAGDALENE NELSON ENOCK MKOCHA**

Bi. Mkocha ana Shahada ya Sayansi katika Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (1979) na Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (1988). Ana uzoefu wa miaka 37 katika sekta ya kilimo, na alikuwa mjumbe wa bodi mbalimbali kama Bodi ya Nyama Tanzania na Kamati ya Ushauri ya VETA. Pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).



**5. PAUL FARAJ KOYI**

Bw. Koyi ana Shahada ya Sayansi katika Elektroniki kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa sasa, Mwenyekiti Mtendaji wa Kampuni ya BN`N Group of Companies. Aidha, aliwahi kuhudumu kama Rais wa Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Mjumbe wa Kamati ya Baraza la Biashara la Tanzania, Mkoa wa Dar es Salaam, Mshauri Mwelekezi wa Biashara Ndogo na za Kati (SME), mkufunzi na mlezi wa vijana. Bw. Koyi pia ni Mjumbe wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania (ERB) kama mhandisi kitaaluma na amesajiliwa na EEU kama mshauri wa ICT kwa miradi ya Kusini mwa Afrika.



**6. LYAMBA JULIUS NG'WANANOGU**

Bwana Ng'wananogu ana Shahada ya Uhasibu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2009) na Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo cha Usimamizi wa Biashara cha Afrika Mashariki na Kati (ESAMI) (2016). Amehudumu kama Mkuu wa Kitengo cha Urejeshwaji wa Madeni toka Benki ya Azania tangu mwaka 2022. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 10 katika taaluma ya Uhasibu, na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).



CamScanner

## KIAMBATANISHO 1 - MAHUDHURIO

**JUMLA YA HISA ZILIZOLIPIWA: 73,077,253**

| SNO | JINA LA MWANAHISA | AINA YA UWAKILISHI |
|---|---|---|
| 1 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | MWAKILISHI |
| 2 | DR. DOROTHY MARTIN MASOZA | BINAFSI |
| 3 | MAJALIWA SHABANI WANYAMALE | BINAFSI |
| 4 | AMAN EDWARD STEPHEN | BINAFSI |
| 5 | QUEEN CHRISTINA RUGAIMUKAMU | BINAFSI |
| 6 | CHRISTOPHER EPHRAIM MWAKISOLE | BINAFSI |
| 7 | MUSTAFA AZAD KARIM | BINAFSI |
| 8 | ALEN STEPHANO MBIMANYA | BINAFSI |
| 9 | TIMBIUS WAMBURA WARYUBA | BINAFSI |
| 10 | LULU SILAS OLANG | BINAFSI |
| 11 | MERIUS ELIUTER NZALAWAHE | BINAFSI |
| 12 | JOEL TIMOTH CHIKOMA | BINAFSI |
| 13 | REVOCATUS BELLE RUMISHA | BINAFSI |
| 14 | ANNA HENRY CHARLES | BINAFSI |
| 15 | PATRICK EDWIN MWAKAJUBE | BINAFSI |
| 16 | GODBLESS GIBSON MINJA | BINAFSI |
| 17 | AHMAD JUMA LAIZER | BINAFSI |
| 18 | JAVAN MUGANDA PERE | BINAFSI |
| 19 | BENNY RUMISHAEL MAKUNDI | BINAFSI |
| 20 | PAUL MATHIAS MAKUNGU | BINAFSI |
| 21 | ABBASI EXPORTS LIMITED | MWAKILISHI |
| 22 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | MWAKILISHI |
| 23 | ZUMBI ELVIS MUSIBA(ADMIN) ELVIS ARISTABLUS MUSIBA (DECEASED) | BINAFSI |
| 24 | NIMROD ELIREHEEMAH MKONO | MWAKILISHI |
| 25 | JAMES MAJUKANO GEGE | MWAKILISHI |
| 26 | AMRAN KHERI BATENGA | BINAFSI |
| 27 | TESE & TECHE ENGINEERING LTD | BINAFSI |
| 28 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD | MWAKILISHI |
| 29 | ELISANTE ELIKANA MURO | BINAFSI |
| 30 | ANTHONY PETER SIYOVELWA (ADMIN) PETER SAID SIYOVELWA(DECEASED) | BINAFSI |
| 31 | TCCIA HQ | MWAKILISHI |
| 32 | BENNY RUMISHAELI MAKUNDI | BINAFSI |
| 33 | DR.TOM GADIEL PENDAEL MAEDA | BINAFSI |
| 34 | MAGDALENA NELSON ENOCK MKOCHA | BINAFSI |
| 35 | TCCIA MOROGORO | MWAKILISHI |
| 36 | LUSANJALA | BINAFSI |
| 37 | JULITHA JOHN MUSHI(ADMIN)ISDORY STANSLAUS MMASSY (DECEASED) | MWAKILISHI |
| 38 | THEOFANIS ALEXANDER SOUTIS | BINAFSI |
| 39 | JANE LAMECK CHACHA | BINAFSI |
| 40 | ERICK ELIZER BALIGE | BINAFSI |
| 41 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI | BINAFSI |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 42 | THOMAS RUGUMBA GHATI | BINAFSI |
| 43 | HUSSEIN KHAMIS SHAABAN | BINAFSI |
| 44 | KANYENYE KISULILA MATANGA | MWAKILISHI |
| 45 | EDGAR MAKWANI MLENGE | BINAFSI |
| 46 | AMINA ISMAIL SHIRNAH | BINAFSI |
| 47 | SHIJA PAUL MTALIS | BINAFSI |
| 48 | OTTO PAUL TEMU | BINAFSI |
| 49 | ISAYA SHAURI MAO | BINAFSI |
| 50 | ISARIA KAWEDI MWENDE | BINAFSI |
| 51 | ARISTIDES JOHN NGOWI | BINAFSI |
| 52 | PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI | BINAFSI |
| 53 | JOAN JAMES MNGODO | BINAFSI |
| 54 | JUBILATE BERNARD MINJA | BINAFSI |
| 55 | BAKA ELECTRICAL CONTRACTOR | MWAKILISHI |
| 56 | VALLERIA POTAMI MANDE | BINAFSI |
| 57 | REHEMA JUMA MUHIMBI | BINAFSI |
| 58 | PROF. LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA | BINAFSI |
| 59 | MR. FORTUNATUS M. MAGAMBO | MWAKILISHI |
| 60 | ERNEST R. KHISOMBI | MWAKILISHI |
| 61 | MR. JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | BINAFSI |
| 62 | MS. MAGDALENE N. E. MKOCHA | BINAFSI |
| 62 | MR. NATHAN EDWARD MNYAWAMI | BINAFSI |



CamScanner

**MKUU WA KUMI NA TISA**

**KUFUNGA MKUTANO**

# KUFUNGA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA



CS CamScanner

LAYOUT & DESIGN: +255 624 400 295 | 717 200 295 | mudithan@mail.com

CamScanner

AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.

**AFRIPRISE INVESTMENTS PLC**
PSSSF Millenium Tower II, 24th Floor
P. O. Box 72678, Dar es Salaam, Tanzania
**Mobile:** +255 753 701 802 | **Email:** info@afriprise.co.tz
www.afriprise.co.tz

CamScanner